**THE SUCCESS PATH EXAMINATION COUNCL (SPEC)**

**Paving the Way to Success**

**102/2** # KISWAHILI

## LUGHA

**Kidato Cha 3**

**MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA KWANZA**

**Muda: Saa 2**

---

**Jina**: ………………………………………………………. **Numbari ya Usajili** …………………

**Shule** ………………………………..………… **Mkondo**: ……………………………….

**Sahihi ya Mtahiniwa** ………………….…………… **Tarehe:** ………………………………..

**Maagizo**

(a) Andika jina lako na nambari yako ya Usajili katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(b) Andika jina ya shule kisha tia sahihi yako katika nafasi ulizoacha hapo juu.
(c) Jibu maswali **yote.**
(d) Maswali yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.
(e) Majibu yote **lazima** iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
(f) Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.
**(g) Karatasi hii ina kurasa 9 zilizopigwa chapa.**
**(h) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawa sawa na kuwa maswali yote yamo**

**Kwa matumizi ya mtahini pekee**

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| Jumla | 80 | |


©2026 The Success Path Examination Council

**1. UFAHAMU** (Alama 15)

*Soma kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Tulipokuwa katika darasa la sita, hali yetu ilikuwa ngumu sana. Hatukuwa na madaftati wala kalamu za kutosha. Shule yetu ilikuwa mbali na nyumbani, takriban kilomita saba, na tulilazimika kutembea kila siku. Nyakati za mvua, tulilowa nguo zote na kufika shuleni tukiwa baridi kali. Hata hivyo, hatukukata tamaa. Mwalimu wetu mkuu, Bwana Odhiambo, alikuwa mwalidi. Alitutia moyo kusoma kwa bidii licha ya matatizo. Alisema, "Mvumilivu hula mbivu." Siku moja, alileta jambo la kushangaza darasani.

Alituambia kwamba alikuwa amepata ufadhili kutoka kwa wazee wawili waliofariki miaka mingi iliyopita. "Ndugu zangu," alianza kwa sauti yenye mashiko, "nimewaalika hapa ili kuwapa habari njema. Wazee hawa waliweka amana katika benki tangu wakati wa ukoloni. Hawakuwa na watoto, na sasa fedha hizo zimetolewa kwa ajili ya wasomi. Nimewatayarishia nyaraka za kuwaweka katika udhamini huo."

Tulishangaa. Juma, rafiki yangu wa karibu, alidondokwa na machozi. Alikuwa na ndoto ya kuwa daktari lakini aliona ni vigumu. Baada ya siku chache, Bwana Odhiambo alitupatia miongozo ya kujaza fomu. Ilitubidi tuwasilishe nyaraka za shule, pamoja na barua za mapendekezo kutoka kwa viongozi wa eneo letu.

Miezi miwili baadaye, tulipokea barua ya kukubaliwa. Sote kumi na wawili tulifanikiwa kupata ufadhili huo. Mwalimu alitukumbatia akituhia na kutuahidi kuwa atatufuatilia maendeleo yetu. Leo hii, nimekwisha maliza chuo kikuu na ninafanya kazi nzuri. Ninapowaza nyuma, naona jinsi mwalimu huyu alivyokuwa kama "kiboko cha maji" hakutuacha tupotee.

(a) Mtunzi anazungumzia changamoto zipi za awali za shule yao? (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………....


©2026 The Success Path Examination Council

(b) Eleza maana ya misemo ifuatayo kwa kuzingatia ufahamu huu:

(i) Mvumilivu hula mbivu. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(ii) Kiboko cha maji. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(c) Mwalimu Bwana Odhiambo alikuwa na sifa gani kuu? Toa mfano. (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(d) Kwa nini Juma alidondokwa na machozi aliposikia habari za ufadhili? (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(e) Ni nyaraka zipi zilihitajika kwa ajili ya ufadhili huo? (alama 3)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(f) Kwa nini mtunzi anasema mwalimu wao alikuwa kama "kiboko cha maji"? (alama 2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………


©2026 The Success Path Examination Council

**2. UFUPISHO** (Alama 15)

*Soma kifungu kifuatasho kisha ujibu maswali.*

Katika safu yangu hii sina lengo la kuzishambulia dini zetu na namuomba

Mungu sana asiniandikie dhambi kutokana na ninayotaka kuyaandika. Lakini nashawishika kuikumbusha jamii yangu ambayo inatufanya watu tuzione dini zetu zinamkandamiza mwanamke. Dini zetu kubwa kama Uislamu na Ukristo zinatuelekeza mwanamke kumheshimu mumewe na kumsikiliza anachosema, lakini kwa yeye kufuata maadili ya dini na si kukuambia uue ukakubali.

Wakati dini inasema utekeleze amri ya mumeo na wao wameelezwa mambo ya kuwafanyia wanawake, ikiwa ni pamoja na kuwaheshima na kuwaridhisha kadri ya uwezo wao.

Kutokana na hilo la amri, wanaume wengi ndio wamechukua kama tiketi ya kunyanyasa mwanamke na hata kumnyima fursa ya kujiendeleza kielimu na hata kufanya shughuli za kuongeza kipato. Unakuta familia ni ya kimaskini, baba hana fedha za kutosha kuihudumia familia yake, lakini baba huyo anataka kujishughulisha

na shughuli yoyote ya kumuingizia kipato kinachoweza kuwasaidia wote na matokeo yake kuendelea kuwepo, kwenye dimbwi la umasikini. Wengine kwa hofu ya kupata changamoto kutoka kwa wake zao wanawakatalia wanawake walio wao kujiendeleza kielimu au kutafuta mwanamke asiyeelimika ili asiweze kuhoji mambo kadhaa ndani ya nyumba.

Hili limebainishwa hivi karibuni na shirika moja lisilo la kiserikali huko kigoma ambapo katika utafiti wao asilimia 90% ya wanawake wa vijijini wanashindwa kutoa hoja kutokana na uelewa wao duni na kutoa sababu ya kuwa hiyo ni kutokana na ukosefu wa elimu, masuala ya kidini yanayomwelekeza mwanamke kufuata amri

za mumewe, mila na desturi kadhaa.

Dini zote zinaeleza wazi umuhimu wa mtu kupata elimu bila kubagua kama ya kiislamu inavyosema; mtu anapata thawabu anapotafuta elimu na anatakiwa aitafute popote bila kujali umbali na hata ikiwezekana kufika China ambapo inaaminika ni mbali.

Sijawahi kuona wala kusikia dini ikisema mwanamke asipate elimu lakini baba zangu na kaka zangu wanaume wanalipotosha hili kutaka kuendelea kumkandamiza mwanamke bila kufikiri kuwa mwanamke ni msaada mkubwa kwao na kwa maendeleo ya taifa lote; ikiwa leo tupo katika harakati za kupata maendeleo na nchi hii hivi kweli tutafanikiwa?

Mapambano ya kuleta maendeleo yaanze katika ngazi ya familia kwa kuondoka kwa ujinga wa kumkandamiza mwanamke ili naye aelimike, aweze kujenga hoja, aweze kujitafutia kipato na mwisho kusaidia katika maendeleo ya familia ambayo kwa njia nyingine ndiyo maendeleo yenyewe ya taifa hili.


©2026 The Success Path Examination Council

(a) Fupisha aya tano za kwanza**. (Maneno 70).**

**Matayarisho**

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………..

**Nakala Safi**

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

(b) Mwanamke anaweza kuendelezwa vipi. Rejelea aya mbili za mwisho. **(Maneno 50)**.

**Matayarisho**

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

**Nakala Safi**

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………


©2026 The Success Path Examination Council

**3. MATUMIZI YA LUGHA NA SARUFI.** **(ALAMA 40)**

(a) Unganisha sentensi hii kwa kutumia 'O' rejeshi. (alama 2)

Wavu umekatika. Wavu ni wao.

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………… ……………………………………………………………………...

(b) Eleza matumizi mawili ya 'ka' na utunge sentensi kwa kila mojawapo. (alama4)

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

(c) Changanua kwa njia ya matawi. (alama4)

Mama anapika na baba anasoma gazeti.

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………

(d) Onyesha viwakilishi katika sentensi zifuatazo kisha ueleze ni vya aina gani. (alama4)

(i) Unamjua vyema kweli?

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

(ii) Hicho wanachokitaka hakipo.

…………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………..

(e) Yakinisha sentensi ifuatayo: (alama1)

Chakula hakipikiki vizuri.

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

(f) Unda nomino moja moja kwa kila kitenzi. (alama4)

(i) Shuku

……………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………....

(ii) Vumilia

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

(iii)Shona

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

(iv)Lia

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

(g) Andika sifa bainifu za sauti: (alama 2)

(i) e-

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

(ii) u-

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

(h) Eleza matumizi mawili ya kiambishi ‘ku’ (alama2)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(i) Tunga sentensi ukitumia maneno haya katika kinyume; (alama2)

(i) Afikiana

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(ii) Sifu

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(j) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao. (alama 3)

N+V+V+T

…………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………...

(k) Onyesha kishazi huru na kishazi tegemezi. (alama2)

Msichana aliyeitwa alikuwa mkorofi.

…………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………...

(l) Eleza maana ya semi hizi: (alama 2)

(i) Kunja jamvi

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(ii) Piga kambi

…………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………...

(m) Ainisha viambishi katika neno lifuatalo: (alama2)

Kilichokitaka

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………


©2026 The Success Path Examination Council

(n) Tunga sentensi ya neno moja yenye mofimu zifuatazo. (alama4)

(i) Nafsi ya tatu umoja.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(ii) Wakati uliopita

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(iii)'O' rejeshi

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

(iv)Mzizi

…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………….................

(o) Nyambua vitenzi hivi kulingana na kauli ya kutendua na kutenda. (alama2)

| **Kutenda** | **Kutendua** | **Kutendama** |
|---|---|---|
| Ficha | | |
| Tanda | | |

**4. FASIHI** **(ALAMA 20)**

(a) Fasihi ina tanzu mbili kuu. Zitaje na utoe mfano kwa kila tanzu. (alama 4)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………..

(b) Eleza dhima tatu za fasihi katika jamii. (alama 6)

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………..